Miji Ya Makimbilio

na

Ellis P. Forsman

Miji Ya Makimbilio

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 11, 2011

Miji Ya Makimbilio

Yoshua 20:1-9

Yoshua 20:1-9, "*Kisha BWANA akanena na Yoshua na kumwambia, nenda wewe na wana wa Israeli, uwaambie haya toeni hiyo miji ya makimbilio, ambayo niliwaambia habari zake kwa mkono wa Musa; ili kwamba mwenye kuua mtu, aliye mwuua mtu awaye yote pasipo kukusudia na pasipo kujua apate kukimbilia kuko; nayo itakuwa ni mahali pa kukimbilia kwenu, kumkimbia huyo ajilipizaye kisasi cha damu. Naye ataikimbilia miji hiyo mmojawapo, naye atasimama hapo penye maingilio ya lango la huo mji, kisha atanena neno lake masikioni mwa wazee wa mji; nao watamtia kwao ndani ya mji na kumpa mahali ili apate kukaa kati yao. Na kama huyo mwenye kujilipiza kisasi cha damu akimwandamia, ndipo hawatamtoa huyo mwuaji kumtia mkononi mwake huyo; kwa sababu alimpiga mwenziwe naye hakujua wala hakumchukia tangu hapo. Naye atakaa katika nji huo, hata hapo atakapo simama mbele ya mkutano kuhukumiwa hata kifo chake kuhani mkuu mwenye kuwapo siku hizo; ndipo yule mwuaji atarudi na kuuendea mji wake mwenyewe na nyumba yake mwenyewe hata mji huo alioutoka hapo alipokimbia. Nao wakaweka Kedeshi katika Galilaya katika nchi ya vilima ya Naftali, na Shekemu katika nchi ya vilima ya Efraimu, na Kiriath-arba (ndio Hebroni) katika nchi ya vilima ya Yuda. Tena ng'ambo ya pili ya Yordani pande za Yeriko upande wa kuelekea mashariki wakaweka Bezeri ulioko nyikani, katika nchi tambarare ya kabila ya Reubeni, na Ramothi katika Gileadi katika kabila ya Gadi, na Golani katika Bashani katika kabila ya Manase. Miji hiyo ndiyo miji iliyoamriwa kwa ajili ya wana wa Israeli wote, na kwa ajili ya mgeni akaaye kati yao ugenini, ili kwamba mtu awaye yote atakayemwua mtu pasipo kukusudia apate kimbilia huko, asife kwa mkono wa mwenye kujilipiza kisasi cha damu, hata hapo atakapokuwa amekwisha simama mbele ya mkutano.*"

Miji ya makimbilio ilitengwa kwa ajili ya sababu tofauti tofauti ya Yuda na Israeli ili kwamba mtu akikimbia kwa sababu ya kutokujua kwamba ameua mtu aweze kutafuta kimbilio pale kwa ndugu na marafiki wa aliyeuawa.

Ebr. 6:18, "*Ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyo imara, sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yale yawekwayo mbele yetu;*"

Dhahiri, mwandishi, Paulo, alikuwa na miji hii ya makimbilio katika akili yake alipoandika mistari hii, maana kila mji unaonekana kuwa na tabia za kanisa.

Kama jinsi mtu alivyomwua jirani yake asivyojua kuwa na uhakika wa usalama kama akipata kuingia katika mji wa makimbilio; vile vile, mtu aliyeko ndani ya Kristo (kanisa) anakimbilio kutoka dhambini na hukumu.

Mwenye dhambi ametenda dhambi dhidi ya Mungu; lakini Yesu ametoa damu yake kwa ajili ya dhambi zetu.

Ulinganifu kati ya miji ya makimbilio na kanisa la Yesu Kristo

KEDESHI inamanisha "takatifu."

Kimsingi kanisa ni kitengo kitakatifu. 1 Petr. 2:9, "*Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu;*"

"*Takatifu*" inapendekeza wazo la "kutengwa." 2 Kor. 6:17, "*Kwa hiyo tokeni kati yao, mkatengwe nao asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha.*"

"Ekklesia" inamanisha "walioitwa nje."

Kol. 1:13-14, "*Naye alituokoa katika nguvu za giaza, akatuamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye tunaukombozi, yaani msamaha wa dhambi;*"

Kwa nini tuitwe kutoka katika dunia kama hatuendi kukaa nje na tutengwe?

Kanisa lipo katika dunia, lakini siyo nje ya dunia.

- Yoh. 17:14-16, "*Mimi nimewapa neno lako; na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wao si waulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Wao si wa ulimwengu kama mimi nisivyo wa ulimwengu.*"

- Rum. 12:2, "*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema , ya kumpendeza, na ukamilifu.*"

"***Wasio safi hawatapita juu yake.***"

Isa. 35:8, "*Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia, nayo itaitwa <u>njia ya utakatifu</u>; wasio safi hawatapita juu yake, bali itakuwa kwa ajili ya watu hao wasafirio, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo.*"

Ni wale watakatifu tu ndiyo watakapokuwapo kwa Kristo atakapokuja tena.

Efe. 5:27, "*Apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.*"

"SHEKEMU" inamanisha "bega."

Unafikiria kitu gani unapofikiri kuhusu bega? "Nguzo" maana bila shaka hujawaikuisikia ikisema, "Weka bega lako kwake."

Kanisa ni "nguzo" la ukweli. 1 Tim. 3:15, "*Lakini nikikawia kuja upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu aliye hai nguzo na msingi wa kweli.*"

- "nguzo na msingi." (Kamusi ya Strong)
- "HEBRONI" "uhusiano," "umoja," au "urafiki."

Tafsiri hizi zote zinaleta wazo la ushirika au umoja. Neno "*ushirika*" inatumika katika Biblia katika mitazamo mitatu.

Ushirika – ulioungana. Fil. 1:3-5, "*Nimshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo, siku zote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza Injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi.*"

Urikiano.

- Mdo. 2:42, "*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.*"
- Mdo. 2:46, "*Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe.*"

Changizo. 2 Kor. 8:1-4, "*Tena ndugu zetu, twawaarifu habari ya neema ya Mungu, waliyopewa makanisa ya Makedonia; maana walipokuwa wakijaribiwa kwa dhiki nyingi, wingi wa furaha yao na umaskini wao uliokuwa mwingi uliwaongezea utajiri wa ukarimu wao. Maana nawashuhudia kwamba, kwa uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao, kwa hiari yao wenyewe walitoa vitu vyao; wakituomba sana pamoja na kutusihi kwa habari ya neema hii, na shirika hili la kuwahudumia watakatifu.*"

“BEZERI” inamanisha “imara” au “ngumu.”

Kanisa lina uimara mgumu, kinga dhidi ya uovu. Katika Kristo na kanisa lake tuna kimbilio kutoka katika hofu na vitisho.

Haiwezekani kwa mishale yenye moto ya shetani kutuingia, au majeshi yaliyoungana ya shetani kudhuru kama tukikaa katika neno lake.

Efe. 6:13-17, “*Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu mpate kuweza kushindana siku ya uovu na mkiisha kuyatimiza yote kusimama. Basi simameni hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa diri ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani; amabayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu;*”

Katika Kristo na kanisa lake tuna kimbilio kutoka katika kifo.

- Mt. 16:18, “*Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*”
- Ufu. 14:13, “*Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya tabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao.*”

“RAMOTHI” inamanisha “urefu” au “wembamba.”

Kanisa la Yesu Kristo lina urefu na sehemu iliyoinuka.

Mt. 5:14, “*Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu yam lima.*”

Hakuna kitengo cho chote duniani iliyoinuka katika makadirio ya Mungu kama kanisa.

Kuna vitengo vingi (kibiashara, kisiasa, kijamii, na kidini) yenye ufahari wa kitaifa; lakini kanisa lina ubora wa kuinuliwa na mvuto wa Mungu.

Hakuna heshima iliyo kuu kama mwanachi anaye nyenyekea katika ufalme wa Mungu. Mt. 11:11, “*Amini, nawaambieni, Hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliyemkuu kuliko Yohana Mbatizaji; walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye.*”

Vile vile wote wanaweza kuwa katika nafasi hii ya heshima.

Watu wengi wamekwenda juu ya mnara ulio katika Washington, D.C. Walipopanda juu yake, wangeweza kuuangalia mji mkuu, na mtazamo wa kuvutia uliopo.

Kanisa la Bwana wetu hakika ni “Ramothi,” yetu au “muinuko.” Njia pekee ya kuweza kutuinua juu ya dhambi, na juu yetu sisi wenyewe, ni kuinuliwa juu katika uwepo wa ukombozi katika Yesu Kristo.

“GOLANI” inamanisha “duara.”

Duara linamanisha ukamilifu, na katika Kristo sisi tumekamilika. Kol. 2:10, “*Na ninyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka.*”

Kanisa ni ukamilifu wa Kristo. Efe. 1:22-23, “*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa ambalo ndilo mwili wake ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika yote.*”

Na Kristo ni ukamilifu wa Mungu. Kol. 2:9, “*Maana katika yeye ukaa ukamilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.*”

Vile vile, katika kanisa la Yesu Kristo una ukamilifu wote wa Mungu na wa Kristo. 2 Yoh. 1:9, “*Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo yeye ana Baba na Mwana pia.*”

Katika Kristo una ukuu wote, mbinu, na kweli ambao hauwezi kupatikana katika kitengo cho chote.

Hupaswi kuwa katika jamii hii au jamii ile au uwezo wa juu ili uwe na mbinu za mema, maana umekamilika katika Kristo. Kol. 2:10, “*Nanyi mmetimilika katika yeye aliyekichwa cha enzi yote na mamlaka.*”

Una kila kitu katika Kristo kuweza kukuinua wewe kama Mkristo. Efe. 1:3, “*Atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho ndani yake Kristo.***”**

Kuwa ndani ya Kristo ni kuwa katika Kanisa lake.

- Gal. 3:27, “*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*”
- 1 Kor. 12:13, “*Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja kwamba tu Wayahudi au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho Mmoja.*”
- Kol. 1:18, “*Naye ndiye kichwa cha mwili yaani cha kanisa; naye ni mwanzo ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.*”

Baadhi ya ukweli kuhusu miji hii ya makimbilio

Njia zilizokuwa zinaendapo zilikuwa laini na iliyonyooka, ipatikanayo kwa wote.

Njia ya utakatifu imenyooka kwa wote.

- Isa. 35:8, "*Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia, nayo itaitwa njia ya utakatifu, wasio safi hawatapita juu yake; bali itakuwa kwa ajili ya watu hao wasafirio, wajapokuwa wajinga hawatapotea katika njia hiyo.*"
- Mika 4:2, "*Na mataifa mengi watakwenda na kusema, njooni twende juu mlimani kwa BWANA, na nyumbani mwa Mungu wa Yakobo; naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake; kwa maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la BWANA litatoka Yerusalemu.*"

Matangazo na vipeperushi ziliwekwa juu ili kuonyesha njia kwa wote.

Mungu ametupatia alama inayotuongoza, ikionyesha katika njia hii kuu ya utakatifu inayoongoza kimbilio katika Kristo Yesu. Zaburi 119:105, "*Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu.*"

Biblia yote imesheheni alama inayonyesha. Agano Jipya liliwaambia Wayahudi kwamba Kristo atakuja.

- Injili Nne zinaonyesha kwamba kweli alikuja.
- Matendo ya Mitume imejaa historia ya uongofu, inayotuambia jinsi ya kuingia katika Kristo.
- Nyaraka za Agano Jipya zinatuambia jinsi ya kuishi maisha ya Kristo na jinsi ya kubaki katika kimbilio la Yesu Kristo.
- Ufunuo wa Yohana inaelezea mji wa nafsi, unaowasubiria wale walio "*osha mavazi yao na kuzifanya nyeupe katika damu ya Mwana kondoo.*"

Miji hii ilifikiwa na watu kutoka sehemu zote za nchi. Vile vile, injili ni kwa watu wote.

- Marko 16:15, "*Akawaambia Enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe.*"

- Tito 2:11-12, "*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za dunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa.*"
- Ufu. 22:17, "*Na Roho na Bibi harusi wasema njoo! Naye asikiaye na aseme, njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure.*"

Miji hii ilikuwa na maji tele na aina zote za mahitaji.

Pia, katika Kristo tuna "*baraka zote za kiroho.*" Efe. 1:3, "*Atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu war oho, ndani yake Kristo;*"

Milango inakuwa wazi usiku na mchana.

- Isa. 55:6-7, "*Mtafuteni BWANA maadamu anapatikana, mwiteni maadamu yu karibu; mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake; na amrudie BWANA, naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa.*"
- Yoh. 6:37, "*Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.*"
- Ufu. 3:7, "*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika; haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufunga wala hapana afungaye; naye afunga wala hapana afunguaye.*"

Kwa vile, mbingu imefanya kila kitu kiwezekane kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu, na kama asipookolewa itakuwa ni kosa lake mwenyewe.